

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA
OFISI ZOTE: +255 736 200911/12

FAX: 255 028 736 200910

E-mail: md@ilemelamc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi,
Manispaa ya Ilemela,
S.L.P 735 – MWANZA

tarehe: 09/02/2022

Namba ya Kotesheni: LGA/159/2021/2022/W/23.

MWALIKO WA KOTESHENI

UPATIKANAJI WA MAFUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA WODI YA WANAWAKE (FEMALE WARD), WODI YA WANAUME (MALE WARD), JENGO LA KUHIFADHIA MAITI (MORTUARY), KICHOMEA TAKA (INCINERATOR), NA JENGO LA UPASUAJI (THEATER).

1. Mwaliko huu wa Kotesheni unafuata Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA kwa Mwaka wa fedha 2021/22. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa kazi za Ujenzi au utekelezaji wa miradi ya HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA katika mwaka wa fedha 2021/2022. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao unatolewa katika mwaliko wa Kotesheni hii.
2. Unalikwa kuwasilisha Kotesheni yako kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kandarasi za ujenzi kama ilivyoelekezwa kwenye Mchanganuo wa makadirio ya kazi ulivyoainishwa.
3. Kotesheni zote zijazwe kikamilifu kwa kuanisha Namba ya Kotesheni kwa ajili ya kazi za:-

Fungu Na.	Maelezo (AINA YA ZABUNI)	NAMBA YA KOTESHENI
1.	Ujenzi wa Wodi ya wanawake (Female Ward).	LGA/159/2021/2022/W/23 - I
2.	Ujenzi wa Wodi ya Wanaume (Male Ward).	LGA/159/2021/2022/W/23 - II
3.	Ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti (Motuary).	LGA/159/2021/2022/W/23 - III
4.	Ujenzi wa kichomea taka (Incinerator).	LGA/159/2021/2022/W/23 - IV
5.	Ujenzi wa jengo la upasuaji (Theatre).	LGA/159/2021/2022/W/23 - V

MASHARTI KWA MUOMBAJI:

- i) Awe Mtanzania (ambatanisha hati kivuli cha Kitambulisho cha Mpiga Kura au cha Taifa au Leseni ya Udereva au Hati ya kusafiria).
 - ii) Awe mwenye ujuzi na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi/ukarabati wa majengo ya serikali usiopungua miaka mitatu ya hivi karibuni (ambatanisha hati ya uthibitisho wa kazi za ujenzi wa majengo ya serikali ambazo umewahi kujenga).
 - iii) Awe na uwezo wa kukamilisha kazi atakayoomba kwa muda atakaopewa.
 - iv) Awe anajua kusoma na kutafsiri vizuri ramani za majengo ya serikali.
 - V) Mwombaji lazima awe na utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kata anayoishi.
 - VI) Cheti cha taaluma ya ufundi ni sifa ya ziada kwa mwombaji.
 - VII) Mwombaji lazima atoke ndani ya Wilaya ya Ilemela au maeneo ya Jirani.
 - VIII) Fundi atakayepata kazi, lazima apatikane/awepo muda wote eneo la kazi.
 - IX) Muombaji anaruhusiwa kuomba fungu zaidi ya moja, lakini kila fungu moja la kazi litatekelezwa na Fundi mmoja tu.
 - X) Dhamani ya kotesheni ni dhamana ya ahadi kwa muombaji (Bid securing declaration).
- 4 Nyaraka za zabuni zinapatikana ofisi ya kitengo cha Manunuzi na Ugavi kwa gharama ya TZS 50,000.00 tu kwa kila jengo isipokuwa kichomea taka kitapatikana kwa TZS 20,000.00. **(Fedha ambayo haitarejeshwa)**
5. Kotesheni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, KATIBU BODI YA ZABUNI HALMASHAURI YA MANISPAA ILEMELA, SLP 735 MWANZA. kabla au saa 5.00 asubuhi ya tarehe 14/02/2022. Ufunguzi wa Kotesheni hizo utafanyika Katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela muda mfupi baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Kotesheni.
6. Kotesheni au sehemu ya Kotesheni ambazo zitawasilishwa kieletroniki au zitawasilishwa nje ya muda uloainishwa hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwaajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yale.


ENG. MODEST J. APOLINARY
MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA.

